**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 05 Mei 2008 mchana**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Eleza vigezo vinne vya kufanikisha uandishi wa insha ya hoja.
2. Toa hoja nne zinazoonyesha faida za kusoma fasihi ya Kiswahili kwa wanafunzi.
3. Tofautisha kati ya methali na nahau kwa hoja nne.
4. Eleza nafasi ya Kiswahili katika kukuza mshikamano wa kitaifa.
5. Taja mambo manne ya kuzingatia mwalimu anapotumia mchezo wa kuigiza darasani.
6. Toa hoja nne zinazoonyesha umuhimu wa tahakiki katika fasihi simulizi.
7. Eleza sifa nne za malengo mazuri ya somo la Kiswahili.
8. Eleza mambo manne ya kuzingatia katika maandalizi ya mtihani wa Kiswahili.
9. Toa hoja nne za kuthibitisha kuwa nyimbo ni njia ya mawasiliano ya kijamii.
10. Taja njia nne za kuhimiza wanafunzi kupenda kusoma vitabu vya ziada.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Jadili mchango wa vitendawili katika kufundisha stadi za lugha.
12. Eleza faida tano za kutumia uchoraji na vielelezo katika kufundisha lugha ya Kiswahili.
13. Kwa hoja tano, eleza umuhimu wa kazi za ushairi shuleni.
14. Eleza hatua nne za kufanikisha mchakato wa ufundishaji wa lugha ya pili.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Eleza sifa tano za mbinu shirikishi za ufundishaji.

16. Toa faida tano za kutoa mazoezi ya mara kwa mara kwa wanafunzi.

17. Eleza mbinu tano zinazoweza kutumika kufundisha sarufi ya Kiswahili kwa ufanisi.

18. Jadili mambo matano yanayoweza kumsaidia mwalimu kuongeza ushiriki wa wanafunzi darasani.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org